JARIDA MTANDAO ROBO YA TATU 2022/2023

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

TOLEO NO 4

www.ubungomc.go.tz/Kitengo cha Mawasiliano Serikalini/Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo




haliuzwi




## UBUNGO NA UWEKEZAJI MKUBWA WA KITUO CHA KIBIASHARA CHA KIMATAIFA

Na Mwandishi wetu

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Makalla aliipongeza Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuifungua Nchi ya Tanzania Kimataifa kwenye masuala ya uwekezaji ambapo wawekezaji wengi kutoka Nchi mbalimbali wanavutiwa kuja kuwekeza Nchini.

Pongezi hizo alizitoa tarehe 19 Januari, 2023 alipotembelea kituo cha biashara cha kimataifa cha "East Africa Commercial and Logistics Center – EACLC" kinachojengwa Manispaa ya Ubungo eneo ilipokuwa Stendi kuu ya Mabasi yaendayo Mikoani.

Mhe. Makalla aliendelea kueleza kuwa kituo hicho kitasaidia kuongezeka kwa fursa mbalilmbali ikiwemo upatikanaji wa ajira, mapato ya Serikali, uchumi na kuitangaza Tanzania Kimataifa Kibiashara kutokana na mwingiliano wa kibiashara wa Nchi mbalimbali.

"Eneo linapojengwa kituo hiki ni la kimkakati na linafaa kwa uwekezaji huo kwasababu ni makutano ya barabara zote hivyo ni rahisi kufikika kutoka sehemu yoyote ndani ya Dar es Salaam, Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Nawapongeza sana Manispaa ya Ubungo kwa kuingia mkataba na wawekezaji wa kituo hicho." Alisema Makalla.

Akifafanua uwekezaji huo Mkurugenzi wa Mradi wa ujenzi wa kituo hicho Ndg. Catty Wang amesema kituo hicho kinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni 2024, una thamani ya dola za kimarekani Milioni 118 sawasawa na pesa za kitanzania Bilioni 271 na utakua na maduka na ofisi zaidi ya 2,000.

Wang ameeleza kuwa, wafanyabiashara wadogo na wakubwa watakuwepo ndani ya kituo hicho pamoja na watengenezaji wa bidhaa mbalimbali kutoka China hivyo wafanyabiashara wa Tanzania na Afrika mashariki kwa ujumla watapata fursa ya kuuza na

Inaendelea Ukurasa wa 2.........



kununua bidhaa zao katika kituo hicho kwani dhamira ya mradi huo ni kuleta bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kwa gharama nafuu.

Nae, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James amesema kuwa, kituo hicho kitakuwa na manufaa makubwa kwa Wilaya ya Ubungo na Taifa kwa ujumla kutokana na umuhimu wake kwani wananchi wengi watapata ajira lakini pia Nchi yetu itapata fedha nyingi za kigeni kutokana na uwepo wa kituo hicho.

Mnamo terehe 16/12/2022 Manispaa ya Ubungo iliingia mkataba na kampuni ya Shanghai Linghang Group Limited ambae ni mwekazaji anaejenga kituo hicho cha Kimataifa cha kibiashara na mkataba huo utafanyiwa marejeo kila baada ya miaka mitatu na kuboreshwa kwa mujibu wa bei za soko.

Aidha, mkataba huo unaeleza kuwa mwekezaji huyo utatakiwa kukabidhi umiliki wa asilimia 100 kwa Manispaa ya Ubungo baada ya muda wa uwekezaji kuisha kwani atakuwa amesharejesha fedha zake za uwekezaji.



# VISHKWAMBI 3354 VYAKABIDHIWA KWA WALIMU WA MSINGI NA SEKONDARI - UBUNGO

Na Mwandishi wetu

Dunia inahama kwa kasi kwenye matumizi ya teknolojia na katika eneo la elimu ni muhimu sana kuendana na teknolojia ili kupata uwiano mzuri wa kuboresha huduma ya elimu.

Hayo yalisemwa Januari 16, 2023 katika ukumbi wa Anazak na mkuu wa wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James wakati anakabidhi vishkwambi 3354 vikiwemo Vishkwambi 2162 kwa walimu wa shule za msingi na Vishkwambi 1192 kwa walimu wa shule za sekondari ili kuongeza tija ya utoaji bora wa elimu.

“Mhe. Rais ana matarajio makubwa sana kwenu. Nendeni mkawasimamie vizuri walimu wenu kwenye matumizi sahihi ya vushkwambi hivyo. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumemuunga mkono Rais kwa vitendo” Alisema James.

Akiongea katika hafla hiyo Mkuu wa Idara ya Elimu sekondari Manispaa ya Ubungo Ndugu Voster Mgina amesema kuwa walimu wote wa Manispaa ya Ubungo watakabidhiwa vishkwambi hivo kila mmoja kwa maelekezo ya kuvitumia kwenye shughuli zao za kikazi ikiwemo kuhifadhi taarifa, kutafuta maarifa pamoja na kufundishia.

Kwa upande wa walimu hao wakuu wamemshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa vishkwambi hivyo na wameahidi kuvitunza na kuvisimamia vizuri ili vilete matokeo yaliyokusudiwa.





## HAKUNA MWANAFUNZI ATAKAYERUDISHWA NYUMBANI KWA KUKOSA MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

Na Mwandishi wetu

"Tunamshukuru Mhe. Rais kwa kuleta elimu bure kwa Shule za Msingi na Sekondari kote Nchini. Na kwa sisi Ubungo tunahakikisha hakuna mwanafunzi yoyote atakayerudishwa nyumbani kutokana na sababu ya kukosa mahitaji muhimu ya Shule"

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James alipokuwa kwenye ziara ya kutembelea Shule za Awali, Msingi na Sekondari za Wilayani humo kwa lengo la kuona mapokezi ya wanafunzi hao katika shule hizo.

Mhe. James aliendelea kusema anamshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuondoa ada ya Elimu ya Sekondari na kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu ili kuwezesha kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia.

Aidha, Mhe James amewaelekeza Walimu ku totoza mchango wa aina yeyote kwa wazazi bila ya kufuata utaratibu wa kuhusisha wazazi na Kamati ya Shule ili kupata lidhaa yao kama miongozo ya elimu inavyotaka.

Nae Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndg. Beatrice Dominic amesema Shule zote za Manispaa ya Ubungo zinaendelea kupokea wanafunzi na zoezi la uandikishaji linaendelea ambapo mpaka sasa wanafunzi walioandikishwa kwa Shule za Serikali kwa darasa la awali ni 2,010 sawa na asilimia 37, darasa la kwanza ni 11,331 sawa na asilimia 83 na kidato cha kwanza ni 15,800 ambayo ni zaidi ya asilimia 50.

Ziara hiyo imekuja leo kufuatia kufunguliwa kwa Shule za Msingi na Sekondari za Umma na binafsi kote nchini kwa mwaka mpya wa masomo 2023 ambapo Mkuu wa Wilaya ametembelea Shule ya Sekondari Mburahati, Shule ya Msingi Amani, Shule ya Sekondari Manzese pamoja na Shule ya Msingi Kimara.



# MAAFISA MAENDELEO YA JAMII NA TASAF WAJENGEWA UWEZO KUHUSU MASWALA YA LISHE

Na Mwandishi wetu

Siku 1000 katika maisha ya mwanadamu ni muhimu Sana, Kila mwanamke anatakiwa kuhakikisha anapata lishe Bora pale tu anapojijua ni mjamzito ili kupata mtoto asiyekuwa na udumavu wala changamoto yoyote ya kiafya.

Hayo yalielezwa tarehe 13 Januari 2023 na Afisa lishe Manispaa ya ubungo Beatrice Mossile alipokuwa anatoa elimu kuhusu maswala ya lishe kwa maafisa maendeleo na Tasaf Manispaa ya ubungo ili waweze kutoa elimu hiyo katika ngazi ya jamii.

Ni muhimu mama kuhakikisha anakula mlo kamili anapojijua ni mjamzito na kuzingatia anapata madini ya chuma ili kuepusha kupata watoto wenye Afya dhaifu, vifo vya watoto wachanga na hata kupoteza maisha wanapojifungua. Alieleza hayo Mossile.

Aliendelea kwa kusema kuwa ni muhimu kuelimishe jamii kuhusu kula Mlo kamili kwa kuzingatia makundi matano, kundi la kwanza ni vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi mbichi, kundi la pili ni mimea na wanyama, la tatu ni mbogamboga, la nne ni matunda na la tano ni mafuta na sukari.

Aidha, Mossile aliendelea kuwakumbusha wakina mama wote pale tu unapojihisi ni mjamzito Kuhudhuria kliniki ni muhimu sana hii kumlinda mtoto aliye tumboni kwani unapowai kufika katika kituo cha Afya inasaidia kupata huduma za Afya ya uzazi mapema ambapo itasaidia katika ukuaji wa watoto na kusaidia kuzaliwa wakiwa na Afya nzuri.

Uzingatiaji na ulaji wa vyakula vyenye ubora kwa Afya husaidia kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza na hata kuweka mwili kuwa imara





Afisa TEHAMA Manispaa ya Ubungo Godfrey Kamugisha (katikati anayetoa maelekezo) akitoa maelekezo kwa wajumbe wa Kamati ya Fedha kuhusu mfumo wa N-Card unaotumika kukatishia tiketi za kuingia ndani ya kituo cha mabasi cha Magufuli Bus terminal.





Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu wakiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.









## KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI YATEMBELEA TAASISI YA KULEA WAZEE

Na Mwandishi wetu

Kamati ya kudhibiti UKIMWI Manispaa ya Ubungo tarehe 27.01.2023 ilitembelea Kituo cha kulea wazee kilichopo Njeteni Kata ya Kwembe kinachoitwa TUSHIKAMANE PAMOJA FOUNDATION kwa lengo la kukitambua kituo pamoja na wazee wanaoishi katika kituo hicho

Akizungumza mwenyekiti wa kamati wa kamati hiyo Mhe. yusuph yenga alisema Halmashauri kwa kushirikiana na Afisa Ustawi itaendelea kuhakikisha wazee hao wanapata mahitaji yao ya muhimu kila siku.

Yenga aliendelea kwa kuwaasa wajumbe kuhakikisha wanatembelea wahitaji hao kwa kuwapelekea mahitaji kadri mtu atakavyo barikiwa na ametoa wito kwa wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kutoa faraja na misaada mbalimbali kwa kituo hicho.

Aidha, Mhe. Yenga aliwapongeza walezi wa Kituo hicho na kuwashukuru na kuwaomba kuendelea kuwajali wazee hao.

“Wazee hawa wanapendeza na wanaonekana wanatunzwa vizuri ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha wazee hao wanapata huduma stahiki” Alisema Yenga.

Akisoma taarifa ya kituo hicho Afisa ustawi wa Manispaa hiyo Ndg. Hellen Samwel alisema kuwa wazee wanaochukuliwa na kituo hicho ni waliofika miaka 60 na kuendelea na kituo hicho kinauwezo wa kuhifadhi wazee 24 ambapo mpaka sasa kituo kina wazee 10, wakiwemo wanaume 6 na wanawake 4.

Hadi sasa Manispaa ya Ubungo ina Jumla ya Kituo kimoja cha kulea wazee ambapo jukumu la Manispaa ni kuhakikisha Kituo hicho kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria , kanuni na taratibu za Nchi yetu.



# RC MAKALLA AKAGUA KIWANDA CHA CHIBUKU KILICHOSIMAMISHA UZALISHAJI TOKA MWAKA 2018

Na Mwandishi wetu

Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam CPA Amos Makalla tarehe 13 Februari, 2023 alifanya ziara ya kutembelea na kukagua kiwanda cha kutengeneza pombe maarufu kama chibuku kilichopo wilaya ya Ubungo Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuona hali ya kiwanda hicho kwa ajili ya kuweka mikakati ya kukifufua.

Akiwa katika kiwanda hicho kilisimamisha uzalishaji wake tangu mwaka 2018, CPA Makalla alipata wasaa wa kujionea samani na vifaa mbalimbali vilivyokuwa vikitumika ndani ya kiwanda hicho.

Akiongea katika ziara hiyo CPA Makalla ameeleza kuwa kusimama kwa kiwanda hicho kunaikosesha Serikali kupata mapato, ukosefu wa ajira kwa vijana pamoja na kupunguza soko la Mahindi ambayo ndio malighafi kuu ya kutengenezea kinywaji hicho.

CPA Makalla aliendelea kusema kuwa kiwanda hicho lazima kifufuliwe na wabia wote wa Dar Brew (Chibuku) ambao ndio wa miliki wa kiwanda hicho akiwemo Jiji la Ilala na Manispaa zote tukutane kwa ajili ya kujadili mstakabali wa kufufua kiwanda hicho kwa maslahi ya Umma.

Aidha, CPA Makalla alieleza kuwa tayari wawekezaji wameeanza kujitokeza kutaka kuwekeza kwenye kiwanda hicho hivyo ni wajibu wetu kutorudi nyuma katika kuhakikisha kiwanda hicho kinafufuliwa.

Ikumbukwe kuwa mwaka 2016 wakati wa kuundwa Wilaya mpya ya Ubungo, kwenye mgawanyo wa Mali na madeni, umiliki wa kiwanda hicho ulihamishiwa Wilaya ya Ubungo.



**Makabidhiano ya Ofisi baina ya Mhe. Kheri James (aliyepo upande wa kulia picha ya juu) aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo na Mhe. Hashim Komba (aliyepo upande wa Kushoto) Mkuu wa Wilaya ya Ubungo wa sasa**





**Taasisi ya Friend's of Samia ikiongozwa na Balozi wao Msanii wa Bongo Fleva Zuwena Mohamed maarufu kama Shilole ilipotembelea Kituo cha Afya cha Palestina kilichopo Kata ya Sinza kwa lengo la kutoa zawadi mbalimbali za siku ya wapendanao kwa akina mama mbalimbali waliokuwa kwenye wodi ya wazazi kituoni hapo.**







## DCC UBUNGO YAPITISHA MAKISIO YA BAJETI YA BIL 109.4 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Na Mwandishi wetu

Kamati ya ushauri ya Wilaya (DCC) ilipitisha Makisio bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ya shilingi 109,449,392,100 kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo. kama sheria ya bajeti ina

Akiongea katika baraza hilo mwenyekiti wa baraza Mhe.Hashimu Komba alisisitiza katika bajeti hiyo vipaumbele ambavyo vinatakiwa kuangaliwa na kuzingatiwa ni kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuboresha miundombinu ya barabara, elimu na afya pamoja na kuboresha mkakati wa utoaji taarifa za Maendeleo.

Aliendelea kupongeza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imeweza kukusanya vizuri mapato mpaka kufikia 103%. Pia Komba alisema kusema kuwa mpaka sasa Hal mashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa mwaka wa fedha 2022 - 2023 imefikia asilimia 51 ya maku sanyo kwa robo mbili ambapo imevuka kiwango cha asilimia 50 kufikia mwezi Disemba 31, 2022.

Aidha wajumbe walipendekeza swala la ukusanyaji wa mapato liweze kusimamiwa vizuri na kusisimamia vyanzo vya makusanyo sambamba na mikopo ya asilimia 10 ambayo hutolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo haijarejeshwa walengwa waweze kusimamiwa na kufuatiliwa waweze kurejesha

Nae Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA Ndg. Amos Maziku wakati akichangia amesema, rasilimali kubwa ya Manispaa ya Ubungo ni watu wake hivyo ameshauri kuandaliwa kwa mipango madhubuti ya kuendelea kujenga uwezo kwa wananchi ili kuongeza tija ya uzalishaji mali kwenye shughuli zao za kila siku.

Katika Majumuisho ya kikao hicho Mhe. Komba ameyapokea mapendekezo yote kwa ahadi ya kuyatekeleza kwa maslahi mapana ya wananchi wa Ubungo.





# TUWAJALI WATOTO NI TAIFA LA KESHO

Na Mwandishi wetu

Ili tuwe na jamii bora yenye upendo na uzalendo ni lazima kila mmoja wetu ajenge utamaduni wa kugusa maisha ya mtoto asiye wa kwake. Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashim Komba alipotembelea kituo cha kulelea watoto yatima cha Huruma Children's Home kilichopo kata ya Goba kwa lengo la kuwafariji.

Akizungumza baada ya kufika kituoni hapo Mhe. Komba alieleza kuwa ilimpendeza kazi yake ya kwanza nje ya ofisi iwe kutembelea kituo hicho kwani watoto hao wanahitaji kufarijiwa kwa maisha wanayoyapitia ya kulelewa kwa maisha wanayoyapitia ya kulelewa bila wazazi.

Katika ziara hiyo Mhe. Komba alikabidhi msaada wa Magodoro 7, Mchele kilo 100, Sukari kilo 25 pamoja na sabuni ili viwasaidie katika mahitaji yao ya msingi kwani kituo pekee hakiwezi kumudu mahitaji yao yote.

Aidha, Mhe Komba alitoa wito kwa wadau na wananchi kwa ujumla kusaidia watoto wanaoishi kwenye vituo hivi ili waweze kufurahia maisha kama watoto wengine. kama ambavyo alivyoonesha mfano Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Ubungo Mhe. Rogart Mbowe alivyoahidi kulipia gharama za maji shilingi 1,800,000/= katika kituo hicho

kwa upande wake Mkurugenzi wa kituo cha Huruma Children's Home Ndg. Dibogo William wakati akieleza historia ya kituo hicho amesema, kituo kilianza mwaka 2006 kikiwa na watoto 16 na hivi sasa kina watoto 26 wawili wakiwa ni wanafunzi wa chuo kikuu ngazi ya shahada na watatu wakiwa ngazi ya stashahada.

"Changamoto kuu za kituo ni upatikanaji wa maji pamoja na kukosa usafiri wa kituo hivyo naomba wadau watakaoguswa watusaidie kutatua changamoto hizi" alisema Dibogo.

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina jumla ya vituo 12 vya kulelea watoto yatima "makao" ambavyo Manispaa ya Ubungo inajukumu la kusimamai vikao hivyo kwa mujibu wa shiria kanuni na utaratibu.



# MADIWANI WA MANISPAA YA UBUNGO WAKUTANA KUPITIA SHERIA NDOGO MPYA

Na Mwandishi wetu

Madiwani wa Manispaa ya Ubungo wameridhia Sheria ndogo mpya za halmashauri hiyo baada ya kusainiwa na mamlaka husika tayari kwa matumizi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo sheria ndogo ya afya na usimamizi wa mazingira.

Madiwani wameridhia kutumika kwa sheria ndogo hizo januari 20, 2023 kwenye mafunzo ya kupata mrejesho wa kusainiwa kwa sheria hizo ili kuwa na ufahamu wa kuanza kutumika katika maeneo yao.

Akiwasilisha sheria ndogo hizo Mkuu wa kitengo cha huduma za sheria wa manispaa hiyo Kissa Mbila amesema kuwa kitengo kimeona ni vema kuwasilisha mrejesho wa sheria hizo kwa waheshimiwa madiwani ili wazipokee na kuzifahamu kabla hazijaanza kutumika.


Kissa alieleza kuwa "Najua Madiwani mlishiriki kwenye mchakato wa utungaji wa sheria hizi lakini tumeona busara kuleta mrejesho huu ili mfahamu lakini pia kuridhia matumizi yake mkiwa kama viongozi na wasimamizi wa Halmashauri"

Akianisha sheria hizo zilizotangazwa kwenye tangazo la serikali la tarehe 15 Julai, 2022, Kissa ametaja sheria ndogo 4 ikiwemo sheria ndogo za afya na usimamizi wa mazingira GN Na 495, sheria ndogo za ada na ushuru GN Na 498, sheria ndogo za ushuru wa huduma GN Na 497 na sheria ndogo za vituo vya mabasi na maegesho ya vyombo vya moto

Wakiongea baada ya kuridhia sheria kuanza kutumia Madiwani wamepongeza kitengo cha sheria kufanya mafunzo hayo na kupendekeza kuanza mchakato wa kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu ili viwe rafiki kwa wananchi wa Ubungo.


Aidha, Madiwani hao wameahidi kwenda kutoa elimu ya sheria hizo kwa wananchi wao na kuwaeleza kuwa sheria hizo zinaanza kutumika rasmi hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kuzingatia sheria hizo.

Ili kuzifahamu kwa undani sheria hizo tembelea kwenye Tovuti ya Halmashauri www.ubungo.go.tz.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
HATUA ZA KUKATA LESENI KWA MFUMO MPYA WA TAUSI
Mfumo huu unapatikana kwenye anwani ya tovuti:
tausi.tamisemi.go.tz
1. USAJILI (REGISTRATION)
Namba ya NIDA (NIN)
Namba ya Simu iliyosajiliwa kwa namba ya NIDA
E - Mail Address
2. MAOMBI YA LESENI (APPLICATION FOR LICENCE)
A. MAOMBI BINAFSI
Tin namba
Mkataba wa pango/ hati ya eneo
Tax Clearance
B. KAMPUNI
TIN namba
Mkataba wa pango/ Hati ya Eneo
Tax clearance
TIN namba ya mwakilishi wa kampuni (care taker)
Memorandum
Certificate of incorporation
Namba ya NIDA ya mwakilishi wa kampuni (care taker)
ubungomanispaa
www.ubungomc.go.tz


HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
MFUMO WA MAPATO
TAUSI
Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, anawatangazia Wananchi wote waliopo katika Wilaya ya Ubungo, kwa sasa unaweza kuomba Leseni ya Biashara, Leseni ya Vileo, na Kulipia Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni kwa Mtandao,
KUPITIA TOVUTI >> tausi.tamisemi.go.tz
Kwa Maelezo zaidi fika Ofisi zetu za Mapato simu 2000 Mawasiliano, Mbezi na makao makuu Manispaa ya Ubungo - Luguruni
Wasiliana na Afisa Biashara wa Halmashauri
+255 713 140 310 II +255 737 700 102


KIBALI CHA UJENZI
KWA MAENEO AMBAYO HAYAJAPIMWA
Mchoro/ Ramani ya Jengo
Nakala ya Kitambulisho cha NIDA, Kura,au Pasi ya Kusafiria
Fomu ya Uhakiki Iliyojazwa kikamilifu
Mkataba wa Mauziano wa Eneo Husika
ubungomanispaa


KIBALI CHA UJENZI
KWA MAENEO YALIYOPIMWA
Uwe na;
HATI YA UMILIKI
MCHORO WA JENGO ULIYOTHIBITISHWA NA MSANIFU MAJENGO
ubungomanispaa


GHARAMA YA VIBALI VYA UJENZI
(Built up Area)
Sq meter 0 - 139.35 = 120,000.00
Sq meter 139.35 - 185.8 = 148,000.00
Sq meter 185.8 - 278.7 = 180,000.00
Sq meter 278.7 - 371.6 = 300,000.00
Sq meter 371.6 - 464.5 = 360,000.00
Sq meter 464.5 - 557.4 = 440,000.00
Sq meter 557.4 - 650.3 = 480,000.00
Sq meter 650.3 - 929 = 1,200,000.00
NOTE; Ada kwa kila 92.90m² itakayoongezeka ni 30,000.00
ubungomanispaa


HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
MIUNDOMBINU BORA MTAANI KWAKO NI MATOKEO YA KODI YAKO
Tembelea Tovuti ya Ubungo Manispaa
www.ubungomc.go.tz

**HALIUZWI**

**OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**S.L.P 55068**

**DAR ES SALAAM**

UBUNGO
**FAHARI YETU**
yetu

**Jarida hili limehaririwa na kusanifiwa na;**
**Joina Nzali**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.**
**Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.**
**Limeandaliwa na;**
**Martha Julius (Afisa Habari-UMC)**
**Twagile Sanga (Afisa Habari- UMC)**
**Filbert Odilo (Afisa Habari- UMC)**


Barua pepe; md@ubungomc.go.tz
Tufuatilie kupitia kurasa za Ubungo Manispaa/ Tovuti: www.ubungomc.go.tz